CRDB BANK

Tunakusikiliza

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 30

Taarifa inatolewa kwamba MKUTANO MKUU WA THELATHINI (30) WA CRDB BANK PLC utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 17 Mei 2025, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba na kwa njia ya kidijitali kuanzia saa tatu kamili (Saa 3.00) asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano**
2. **Kuridhia Dondoo**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Tisa (29) uliopita**
4. **Kujadili yatokanayo na kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Tisa (29)**
5. **Kujadili na kupokea Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2024**
    - 5.1 Taarifa ya Wenye Dhamana ya Uongozi.
    - 5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2024.
    - 5.3 Gawio kwa mwaka 2024.
6. **Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi**
7. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu**
8. **Mabadiliko ya vifungu Na. 88, 92, 94.2, 94.3, 98 na 167 vya Katiba ya Benki**
9. **Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi**
    - 9.1 Kuchagua Mjumbe mmoja (1) Huru wa Bodi
    - 9.2 Kuchagua Mjumbe mmoja (1) wa Bodi atakayewakilisha kundi la wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%).
    - 9.3 Kuchagua Wajumbe watatu (3) wa Bodi watakaowakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja (1%).
10. **Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa**
11. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti**
12. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao**
13. **Kufunga Mkutano**

**MAELEZO**

1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe **07/05/2025** na litafunguliwa tena tarehe **08/05/2025***
2. *Mapendekezo kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 10 yatumwe na yamfikie Katibu kabla ya **Alhamisi tarehe 01/05/2025 saa 10.00 jioni***
3. *Makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana matawini na yanaweza kuchukuliwa kuanzia **tarehe 09/05/2025**, vinginevyo yatapatikana Arusha kwenye ukumbi wa mkutano tarehe **16 hadi 17 Mei 2025.** Pia makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana kwenye tovuti ya benki www.crdbbank.co.tz kuanzia tarehe **09/05/2025***
4. *Wanahisa wanaotaka kuhudhuria Mkutano Mkuu watajigharamia usafiri na malazi*

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatavyo:

**Katibu**
**CRDB Bank Plc**
**S. L. P. 268**
**Dar-es-Salaam**
**Barua pepe:** shares_unit@crdbbank.co.tz
**Namba ya kiganjani:** 0755 197 700
**Namba ya WhatsApp:** 0767 757 215

KWA IDHINI YA BODI

Pascal Mihayo
**KATIBU**

16 Aprili, 2025